EAST AFRICAN COMMUNITY

EAC Close
P.O. Box 1096
ARUSHA, TANZANIA

Tel: +255-27-2162100/14
Fax: +255-27-2162102/2162191
E-mail: eac@eachq.org

OFFICE OF THE SECRETARY GENERAL

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUFUATIA MAZUNGUMZO KATI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC) NA TAASISI ZA SEREKALI NA WADAU MBALIMABLI KUHUSIANA NA UCHAGUZI MKUU WA JAMHURI YA BURUNDI 2020

08TH FEBRUARI 2020

Ndugu Waandishi wa Habari

- Nachukua fursa hii kuwasalimu na kuwashukuru kwa kuitikia wito wetu na kuhudhuria kikao hiki cha waandishi wa habari.

- Napenda pia kuwashukuru kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kufanya katika kuwafahamisha na kuwaelimisha wananchi juu ya faida za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

- Kama mnavyojua mwaka huu wa 2020 utakuwa mwaka wa matukio mengi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwani mzunguko wa uchaguzi umeanza, na utaendelea kwa kipindi cha miaka mitatu. Jamhuri ya

Burundi itafanya uchaguzi wake mwezi Mei mwaka huu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya uchaguzi wake mwezi Oktoba mwaka huu, Jamhuri ya Uganda itafanya uchaguzi wake mwaka 2021, na Jamhuri za Kenya na Rwanda mwaka 2022.

- Ibara ya 124 ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inatambua umuhimu wa amani na usalama ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya. Kifungu hiki pia kinaelezea kwa upana njia za utekelezaji ili kuwa na mazingira salama ndani ya Jumuiya.

- Mkataba huo pia unaipa Sekretariat ya Jumuiya ya Afrika Mashariki jukumu la kusimamia mchakato wa chaguzi zote katika nchi wanachama, kulingana na Katiba za nchi husika. Jukumu hili linazingatia kutambuliwa kwa utawala bora kama moja wapo ya kanuni za msingi zinazosimamia na kufanikisha malengo ya Jumuiya.

- Ni kulingana na msingi huu Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwa ikipeleka Misheni za Waangalizi wa Uchaguzi (EAC-Election Observer Missions) kwa wanachama wake wote pale wanapokua katika mchakato wa uchaguzi. Hii ikiwa ni sambamba na kanuni ya kukuza utawala wa demokrasia katika Jumuiya.

- Uangalizi wa chaguzi za EAC unaongozwa na kanuni za kimataifa na za kikanda, ikiwa ni pamoja na viwango vya juu vya utawala, demokrasia, haki za binadamu na uhuru. Viwango vya Uangalizi wa Uchaguzi vimeainishwa katika kanuni za Jumuiya ya Afrika za Uangalizi na Tathmini za Uchaguzi ya mwaka 2012, ambayo pamoja na mambo mengine huweka wigo wa Waangalizi wa uchaguzi. Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inajiandaa kuleta Burundi Waangalizi wa Uchaguzi kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mei 2020.

- Misheni ya Waangalizi wa Uchaguzi hawa itafuatilia mchakato mzima wa uchaguzi, itatoa tathmini iliyo na usawa na kamili. Waangalizi hao watabaini changamoto, na fursa ambazo zinaweza kujumuishwa kama mafunzo bora katika mchakato wa uchaguzi na Bodi za Usimamizi wa

Uchaguzi (Electoral Management Bodies) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

- Tuna tarajia Waangalizi wa Uchaguzi wa Jumuiya (EAC) wataongeza imani ya wananchi wa Burundi katika mchakato wa uchaguzi wao; wata hamasisha wapiga kura na vyama vya siasa kushiriki katika mazingira huru, na ya haki; pasipo na vitisho wala vurugu.

- EAC italeta Waangalizi wa Uchaguzi watakao shirikiana na vyombo vya Usimamizi wa Uchaguzi na wadau muhimu kuhakiki mazingira ambayo uchaguzi umeandaliwa. Waangalizi wa muda mrefu watafuatilia mchakato mzima – kabla ya uchaguzi, kipindi cha kupiga kura, na hali kadhalika baada ya uchaguzi. EAC pia itatuma Waangalizi wa muda mfupi ambao watatathmini uchaguzi siku ya kupiga kura.

- Waangalizi hawa watajumuisha wawakilishi kutoka nchi wanachama, Mabaraza ya Usimamizi wa Uchaguzi kutoka nchi wanachama, Bunge la Afrika Mashariki (East African Legislative Assembly), Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara za Afrika Mashariki, Taasisi za Haki za Binadamu, Asasi za Kiraia na taasisi zingine.

- Wajumbe kutoka Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekuwa jijini Bujumbura kwa takriban wiki sasa, wakifanya mashauriano na wadau mbali mbali. Kusudi kubwa la mashauriano haya lilikuwa kutathimini hali ya maandalizi ya uchaguzi katika Jamhuri ya Burundi. Pia tumechukua fursa hii kuandaa msingi wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki watakao kuja hapo baadaye.

- Mashauriano yetu yamejumuisha mikutano na tume ya Uchaguzi (CENI) ya Burundi, Mawaziri mbali mbali na vyama vya siasa vilivyosajiliwa nchini Burundi.

- Wakati wa mashauriano yetu, tumejadiliana mambo mengi kuhusu maandalizi ya uchaguzi. Tuna imani uchaguzi huu utakuwa wenye amani na mafanikio.

- Tunaipongeza sana Serikali ya Burundi kwa maadalizi makubwa ambayo yamekwisha fanyika. Tumebaini ya kwamba maandalizi yamekamilika na kuna mazingira yatakayo wezesha uchaguzi kufanyika kwa amani.

- Tumefurahi pia kuona vyama vya siasa karibu vyote nchini Burundi viko tayari kushiriki katika uchaguzi, na vyama kadhaa tayari vimekwisha teua wagombea wao. Pia tumeambiwa kuna group la WhatsApp ambalo wadau wote wanashiriki kuwasiliana.

- Mashauriano yetu yamepanua uelewa wetu juu ya hali ya maandalizi ya uchaguzi nchii Burundi. Sasa tuko tayari kuwaleta Waangalizi wa Uchaguzi.

- Kama Jumuiya ya Afrika Mashariki tuna ahidi ushirikiano na serkali na kama utahitajika msaada wetu katika kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani na utulivu na kwamba utakuwa huru na wa haki.

- Tunatumaini vyombo vya habari vya Burundi na nje ya Burundi vitasaidia sana kulinda na kuienzi amani iliyopo Burundi, na kuhakikisha kwamba uchaguzi utafanyika kwa amani; na Warundi wataendelea na maisha yoa kwa amani hata baada ya uchaguzi.

ASANTE SANA